## *Je,* ni utaratibu gani wa kuingia kwenye muungano na ni nini hufanyika kwa vyama vya kisiasa ambavyo vimeungana?

Sheria (PPA) inaeleza kwamba pale ambapo Vyama vya Kisiasa vinakusudia kuungana, huweka kwa Msajili wa Vyama vya Kisiasa nyaraka zifuatazo:

- ***Makubaliano yaliyothibitishwa ya muungano.***
- ***Nyaraka zinazoonyesha kuwa sheria na taratibu za vyama vya kisiasa vinavyoungana zimefuatwa.***
- ***Kumbukumbu za mkutano wa baraza simamizi la vyama vya kisiasa vinavyounganisha kuidhinisha kuungana.***

Chama cha kisiasa basi kinapokea barua ya uthibitisho kutoka kwa Msajili na cheti cha usajili kamili kinatolewa. Vyama vilivyoungana basi hutolewa katika sajili zao, mali na madeni huhamishwa kwa chama kipya.

Maelezo zaidi kuhusu miungano ya vyama vya kisiasa kwenye Mwongozo wa Miungano ya Vyama vya Kisiasa uliopo kwenye tovuti ya ORPP, **https://orpp.or.ke/mergers_coalitions_coalition_political_parties/.**

## *Ni nini* maana ya mseto wa vyama vya kisiasa?

Mseto ni wakati ambapo vyama viwili au zaidi vinaungana kwa madhumuni ya kufuata lengo moja. Kuna aina mbili za miseto:

- ***Miseto ya kabla ya uchaguzi***
- ***Miseto ya baada ya uchaguzi***

## *Ni maana* ya mseto chama cha kisiasa?

Mseto chama cha kisiasa ni mseto uliosajiliwa kama chama na umeondolewa kisheria mahitaji ya kifungu cha 5 na 6 cha Sheria ya Vyama vya Kisiasa.

Maelezo zaidi kuhusu mseto vyama yapo katika Mwongozo wa Miseto ya Kabla na Baada ya Uchaguzi kwenye tovuti, **https://orpp.or.ke/mergers_coalitions_coalition_political_parties/.**

## *Ni nini* tofauti baina ya mseto na muungano?

Mseto unatofautiana na muungano, katika mseto, vyama hivyo vya kisiasa licha ya kuundwa ushirikiano wao, huhifadhi vitambulisho huru vya kisheria unaodhihirika katika uongozi wao, katiba, wanachama kati ya vitambulisho vingine vya ushirika.

## *Je,* ni nini mchakato wa kuleta mabadiliko katika vyama vya kisiasa?

Chama cha kisiasa kinachokusudia kubadilisha au kurekebisha (katiba yake, kanuni, cheo, jina au anwani ya maafisa, eneo la ofisi kuu au ofisi ya kaunti, alama au kauli mbiu, anwani ya eneo lazima kiwasilishe kwa maandishi kwa mfumo uliowekwa kwa Msajili mabadiliko yaliyokusudiwa ndani ya muda uliowekwa (kifungu cha 20 cha PPA).

## *Je,* vyama vya kisiasa hutatua vipi mizozo inapoibuka?

Katiba za vyama vya kisiasa zinaviihitaji vyama viwe vimeweka utaratibu wa ndani wa utatuzi wa migogoro ndani ya miundo wao. Hii mara nyingi hupatikana katika katiba za vyama vyao na / au sheria za uteuzi. Vyama vya kisiasa kwa hivyo, vinapaswa kuanzisha mchakato wa utatuzi wa mizozo ndani ya utaratibu huu wa ndani uliowekwa. Wakati ambapo mzozo haujasuluhishwa kwa ndani, chama cha kisiasa au wanachama wao wana chaguzi anuwai. Hizi ni:

- ***Jopo la Migogoro ya Vyama vya Kisiasa (PPDT).***
- ***Kamati ya Usuluhishi wa Migogoro ya Uteuzi (IEBC).***
- ***Mahakama Kuu.***

## *Jopo* la Migogoro ya Vyama vya Kisiasa (PPDT) ni nini?

Mahakama ya Migogoro ya Vyama vya Kisiasa (PPDT) ni chombo cha kimahakama kilichoanzishwa chini ya Sheria ya Vyama vya Kisiasa. Jopo hili lina mamlaka ya kusikiliza:

- *Migogoro kati ya wanachama wa chama cha kisiasa.*
- *Migogoro kati ya mwanachama wa chama cha kisiasa na chama cha kisiasa.*
- *Migogoro kati ya vyama vya kisiasa.*
- *Migogoro kati ya mgombea huru na yule wa chama cha kisiasa.*
- *Migogoro kati ya washirika wa muungano.*
- *Rufaa kutoka kwa maamuzi ya Msajili wa Vyama vya Kisiasa.*

## *PPLC* ni nini?

Sheria ya Vyama vya Kisiasa (PPA), 2011, Sehemu ya 38 inaanzisha Kamati ya Uhusiano ya Vyama vya Kisiasa (PPLC) katika ngazi ya kitaifa na kaunti. Kamati hii inashirikisha Afisi ya Msajili wa Vyama vya Kisiasa, Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka na vyama vyote vya kisiasa vilivyosajiliwa kikamilifu. Jukumu lake ni kutoa jukwaa la majadiliano kati ya ORPP, IEBC na vyama vya kisiasa.

## *Je,* vyama vya kisiasa vinafadhili vipi shughuli zao?

Vyama vya kisiasa vinapaswa kupata fedha zake kutoka kwa vyanzo halali. Vyanzo hivi ni pamoja na: ada ya uanachama, michango ya hiari, michango / wasia / misaada halali, mapato ya uwekezaji. Vyama vya kisiasa vinavyofikia kiwango kilichotolewa chini ya kifungu cha 25 (2) ya PPA, 2011 vinastahiki ufadhili kutoka kwa Hazina ya Vyama vya Kisiasa. Chama cha kisiasa kitaweka wazi kwa Msajili maelezo kamili ya fedha zote au vyanzo vingine vya fedha zake.

## *Maafisa* wa chama ni akina nani na ni vigezo gani vinafuatwa katika kuwachagua?

Maafisa wa chama ndio wasimamizi wa vyama vya kisiasa. Vigezo vya kuchagua viongozi vimeainishwa katika katiba ya chama na / au kanuni kulingana na ratiba ya pili ya PPA, 2011.

## *Je,* vyama vya kisiasa vina afisi za magatuzi?

Chama cha kisiasa kinapaswa kudumisha afisi za matawi zinazofanya kazi katika kaunti angalau 24 ambazo lazima ziashirie hadhi kama ile ya afisi kuu.


**Lion Place, Ghorofa ya 1, 2 na 4, Barbara ya Waiyaki, Barabara ndogo ya Karuna.**

**Ofisi za Kaunti: https://orpp.or.ke/offices/**

**+254 20 402 2000 / +254 772 281 357**

**Sanduku la Posta 1131 - 00606 Nairobi, Kenya**

**info@orpp.or.ke**

**www.orpp.or.ke**

**ORPPKenya** **@ORPPKenya** **ORPPKenya**


REPUBLIC OF KENYA

OFFICE OF THE REGISTRAR OF POLITICAL PARTIES
ORPP
Strengthening Political Parties

# AFISI YA MSAJILI WA VYAMA VYA KISIASA



# MASWALI YANAYOULIZWA MARA KWA MARA

## *Ni nini* wajibu na uongozi wa Afisi ya Msajili wa Vyama vya Kisiasa?

Afisi ya Msajili wa Vyama vya Kisiasa ni Afisi huru kuzingatia Kipengee cha 260 cha Katiba ya Kenya, 2010 na iliyobuniwa na kifungu cha 33 cha Sheria ya Vyama vya Kisiasa, 2011. Wajibu wake ni: kusajili, kudhibiti na kusimamia hazina ya Vyama vya Kisiasa. Afisi hii inao wafanyakazi weledi na wazoefu ambao humsaidia Msajili wa Vyama vya Kisiasa kutekeleza majukumu ya Afisi. Zaidi, katika kutekeleza majukumu yake, Afisi hushirikiana na wadau wengine wa serikali na nyanja zisizo za kiserikali.

## *Ninawezaje* kusajili chama cha siasa?

Sheria ya Vyama vya kisiasa, 2011 (PPA) ikiambatanishwa na Kanuni za Vyama vya Kisiasa (Usajili), 2019 inatoa ufafanuzi, mahitaji na masharti ya usajili wa vyama vya kisiasa. Usajili ni hatua mbili:

Usajili wa muda. Wanaonuia kusajili vyama wanahitajika kutimiza yafuatayo:

- *Kutafuta jina: Jina, alama na rangi, kulingana na Kifungu cha 91 cha Katiba ya Kenya na kifungu cha 8 cha PPA.*
- *Kuwasilisha katiba ya chama kuzingatia kifungu cha 9 cha PPA;*
- *Kuwasilisha kumbukumbu za mkutano wa kwanza wa waanzilishi wa chama.*
- *Ambatisho lililotiwa sahihi la ahadi ya kutii Kanuni za Maadili ya Vyama vya Kisiasa.*
- *Kuwasilisha kanuni za uteuzi na uchaguzi.*
- *Wasilisha ombi kwa maandishi katika fomu iliyotengwa.*
- *Lipa ada iliyowekwa (Shilingi 100,000.00) inayolipwa kwa njia iliyotengwa ya kulipa.*

Mahitaji ya Usajili kamili:

- *Kupata wanachama wasiopungua 1000 waliosajiliwa kama wapiga kura kutoka zaidi ya kaunti 24 za Kenya; Hawa wanapaswa kudhihirisha sura ya kimaeneo na makabila tofauti; usawa wa kijinsia na uwakilishi wa vikundi maalum ikiwa ni pamoja na wachache na waliotengwa*
- *Uundaji wa viongozi wa chama uthibitishe sura ya kimaeneo na makabila tofauti; usawa wa kijinsia na uwakilishi wa vikundi maalum;*
- *Viongozi wa chama wathibitishe kukidhi matakwa ya Sura ya 6 ya Katiba ya Kenya; na Sheria ya Uongozi na Uadilifu, 2012.*

Wasilisha kwa Msajili katika muundo uliowekwa:

- *Orodha ya majina, anwani na maelezo ya wanachama wake wote.*
- *Makao ya afisi yake kuu iliyosajiliwa na matawi ya chama katika angalau kaunti 24.*
- *Uainishaji wa data kwa misingi ya makundi maalum.*
- *Ahadi ya kutii kanuni za Maadili ya Vyama vya Kisiasa.*
- *Ada iliyowekwa (Shilingi 500,000.00) inayolipwa kwa njia iliyotengwa ya malipo.*

***Kumbuka: Angalia tovuti ya ORPP, https://orpp.or.ke/, kwa maelezo kuhusu usajili wa vyama vya kisiasa kidijitali.***

## Ni malipo gani mbali mbali za kusajili chama cha kisiasa?

Ada zinazolipwa kusajili chama cha kisiasa:

- *Ada ya ukaguzi wa jina–Shilingi mia tano (500.00)*
- *Usajili wa muda –Shilingi elfu mia moja (100,000.00)*
- *Usajili kamili – Shilingi elfu mia tano (500,000.00)*

## Hivi sasa kuna vyama vingapi vya kisiasa vimesajiliwa?

**Sheria ya Vyama vya Kisiasa, 2011 inahitaji Msajili wa Vyama vya Kisiasa kuweka rejesta ya vyama vya kisiasa vilivyosajiliwa. Angalia orodha ya sasa ya vyama vya kisiasa vilivyosajiliwa kupitia wavuti wa ORPP, https://orpp.or.ke/.**

## Ni mbinu gani ORPP imeweka kuzuia usajili usiofaa wa wanachama na kulinda data ya kibinafsi?

Chama cha kisiasa kinahitaika kupata idhini kwa njia zilizotengwa kwa mtu yeyote kinachokusudia kusajili kama mwanachama. Kati ya mbinu hizi ORPP imeweka ni kubidi vyama vya kisiasa kutuma ujumbe mfupi kwa watu wanakusudiwa kusajiliwa kama wanachama kabla ya kusajiliwa.

Kuhusu kulinda data ya kibinafsi, ORPP kwa ushirikiano na Afisi ya Ulindaji Dat (ODPC) imesambaza maelekezo kuhusu swala hili kwa vyama vya kisiasa kuvisaidia kuweka stakabathi na data kulingana na sheria zilizopo.

## Je, ni jinsi gani ya kujisali, kujiuzulu au kutambua wanachama wangu kwenye chama cha kisiasa?

Kunazo njia mbili; ya Ana kwa Ana na ya Kidijitali.
**Ana kwa Ana:** Kujiuzulu, wasilisha notisi, barua au barua pepe kwa chama husika ulichosajiliwa ikiambatanishwa na nakala ya kitambulisho au pasipoti. Wasilisha nakala hiyo hiyo kwa Msajili wa Vyama vya Kisiasa katika afisi ya ORPP kuu au afisi za gatuzi. Angali tovuti, https://orpp.or.ke/, kwa mbina ya kujiunga kama mwanachama au kutambua uanachama.

**Njia ya Kidijitali:** Unaweza kupata huduma za uanachama kupia: *509# kupitia mtandao wowote kwenye simu ya rununu, Integrated Political Parties Management System (IPPMS) au tovuti ya eCitizen. Pata maelezo zaidi kwenye: https://orpp.or.ke/online-services-2/

***Kumbuka: Afisi ya Msajili wa Vyama vya Kisiasa haisajili wanachama katika vyama vya kisiasa bali inathibiti sajili wa wanachama kama zinavyowasilishwa na vyama vya kisiasa vilivyosajiliwa.***

## Je, mtu anaweza kuwa mwanachama wa chama zaidi ya kimoja?

Hapana. Mtu anaweza tu kuwa mwanachama wa chama kimoja cha kisiasa. Mara tu jina la mtu limeingizwa kwenye rejista ya uanachama wa chama cha kisiasa, mtu huyo anakuwa mwanachama wa chama hicho hadi wakati ambapo atakapojiuzulu au ametolewa kuwa mwana chama husika.

## Je, ni njia zipi za kuacha kuwa mwanachama wa chama cha kisiasa?

1. **Kujiuzulu kwa hiari** - kwa kutoa barua ya kujiuzulu kwa chama na / au Msajili.
2. **Kutolewa** - kupitia mbinu za chama uliowekwa.
3. **"Kuonekana"** - ambapo mwanachama anahusika kwa njia inayoonyesha kuwa yupo katika chama cha kisiasa au anakiunga mkono, mbali na chama ambacho kiko katika mseto wa vyama.
4. **Sababu za kiasilia** - mtu anapofariki.

## Ni nini maana na kazi ya "IPPMS" katika usimamizi wa rekodi za vyama vya siasa?

IPPMS ni jukwaa la teknolojia mtandaoni uliobuniwa na Afisi ya Msajili wa Vyama vya Kisiasa. Inachangia kusimamia na kudumisha rekodi za vyama vya kisiasa katika hifadhidata. Watumiaji walioidhinishwa kutoka vyama vya kisiasa wanao uwezo wa kutumia wenyewe jukwaa hili kupitia IPPMS katika kusimamia na kuwasilisha rekodi za uanachama kwa Msajili. Baadhi ya moduli zake ni kama: Ukaguzi wa uanachama na kujiuzulu chamani; upakiaji mwingi wa data ya uanachama; usimamizi wa mali ya vyama vya kisiasa na maafisa; rejista ya vyama vya kisiasa (Orodha ya vyama vya kisiasa vilivyosajiliwa na maelezo yao). Kutuma maombi ya usajili wa vyama vya kisiasa angalia tovuti yetu (https://orpp.or.ke/) kwa maelezo zaidi.

## Chama cha kisiasa kinapaswa kudumisha rekodi zipi?

Chama cha kisiasa kina wajibika kudumisha rekodi na sahihi katika ofisi yake kuu na ofisi za kaunti kwa muundo uliowekwa. Rekodi hizi ni pamoja na rejista ya wanachama wake; nakala ya katiba; kanuni za uteuzi na uchaguzi;sera na mipango ya usimamizi na usimamizi; vitabu vya hivi karibuni vya hesabu zilizokaguliwa; mali na hesabu ya dhima kati ya rekodi zingine kama ilivyoainishwa katika sehemu ya 17 ya PPA.

Rekodi zinapaswa kupatikana na wanachama wao (zinaweza kuwa kwa ada iliyowekwa). Msajili anaweza kusababisha sababu za ukaguzi wa rekodi za vyama vya kisiasa kupitia utaratibu ulioainishwa chini ya kifungu cha 18 cha PPA.

## Je, katika mazingira yepi ambapo jina la usajiliwa chama linaweza kukataliwa?

Kulingana na kipengee cha 8 cha PPA, jina linalopendekezwa laweza kukataliwa ikiwa:

- *Sio la adabu au lakera.*
- *Ni refu kupita kiasi.*
- *Ni jina, au akronimu/ufupisho wake ni la chama kingine cha kisiasa ambacho tayari kimesajiliwa.*
- *Wakati ambapo jina linashabihiana kwa ukaribu na jina lingine au ufupisho wa jina la chama kingine cha kisiasa kilichosajiliwa tayari au taasisi nyingine yoyote iliyosajiliwa kisheria.*

## Ni njia ipi ya kudhibitishwa mgombea huru?

Kuwasilisha ombi lako kwa njia ya ana kwa ana au kidijitali. Baadhi ya mahitaji mgombea huru anahitajika kuwasilisha ni:

- *Barua ya ombi la kuidhinishwa.*
- *Nakala ya kitambulisho cha kitaifa.*
- *Ada ya shilingi mia tano (500).*

Kwa ufanisi, mgombea anahimizwa kuwasilisha alama (fomati iliyochapishwa kwa kielektroniki) wanayotarajia kutumia kwa madhumuni ya uthibitishaji na IEBC.

Maombi kupitia njia ya kieletroniki ni kupia IPPMS, pata maelezo kwa kina kuhusu mchakato huu yamo katika tovuti ya **https://ippms.orpp.or.ke/.**

## Je, mtu anaweza kuwa mgombea huru bado akiwa mwanachama wa chama cha kisiasa?

**La.** Katiba imeweka bayana kwamba mtu anaweza kugombea kama mgombea huru ikiwa yeye sio mwanachama wa chama chochote cha kisiasa miezi mitatu kabla ya siku ya uchaguzi mkuu. Mwanachama wa chama cha kisiasa anaweza kugombea uchaguzi kama mgombea huru baada ya kujiuzulu kulingana na taratibu za kujiuzulu.

## Je, ni haki na muda gani kwa chama cha kisiasa kilichosajiliwa kikamilifu kushiriki katika uchaguzi?

Mara tu chama cha kisiasa kinapopata cheti cha usajili kamili kinapata hadhi ya kishirika inayowezesha kiendeshe shughuli zake kisheria kama shirika.
Chama kinawajibika:

- *Kuweka wagombea wake katika uchaguzi mkuu na chaguzi ndogo kilingana na muda uliwekwa na kanuni za Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka (IEBC). Ikiwa chama kitashindwa kuweka mgombea yeyote kwenye uchaguzi kuu mara mbili mfululizo, kitafutiwa usajili wake.*
- *Kuwasilisha tamko kwa maandishi mali na deni zake chini ya siku 60 kutoka tarehe ya usajili kamili.*

## Je, chama kilicho na usajili wa muda chaweza kuwasilisha mgombea kwenye uchaguzi?

Hapana. Chama cha kisiasa kilichosajiliwa kwa muda kimekatazwa kushiriki katika shughuli zozote za uchaguzi, pamoja na kuweka wagombea, kumpigia kampeni au kumpinga mgombea yeyote au kufanya mikutano yoyote ya hadhara.

Hata hivo, kina haki ya kutangaza chama kupitia njia zilizoidhinishwa na kutafuta ulinzi wa usalama na msaada kwa shughuli zake.

## Je, muungano wa chama cha kisiasa ni nini?

**"Muungano"** wamaanisha vyama viwili au zaidi vya kisiasa kuunganisha shughuli zao na kuwa chama kimoja cha kisiasa. Sheria ya Vyama vya Kisiasa, 2011 inawezesha muungana wa vyama vya kisiasa ambapo vyama huvunjwa kwa minanjili ya kuunda chama kipya.